

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**  
**OFISI YA RAIS**  
**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

**MKOA WA RUKWA**  
**Anuani ya Simu: "REGCOM"**  
**Simu Na: 025-2802318/2802137**  
**Nukushi. (025) 2802217**  
Barua pepe: ras@rukwa.go.tz



Ofisi ya Mkuu wa Mkoa,  
1 Barabara ya Mkoani,  
S.L.P. 128,  
55180 Sumbawanga,  
**RUKWA.**

## **TAARIFA KWA UMMA**

### **MITIHANI YA KUMALIZA ELIMU YA MSINGI 2024**

Kuanzia tarehe **11 Septemba 2024** wanafunzi wa darasa la saba nchini kote wataanza mitihani ya kumaliza elimu ya msingi ambao unatarajiwa kukamilika tarehe **12 Septemba 2024**.

Katika Mkoa wa Rukwa jumla ya watahiniwa **27,074** wataungana na watahiniwa wengine nchini kufanya mitihani huo wa darasa la saba.

Ambapo jumla ya watahiniwa **27,074** kati yao wasichana ni **15,236** na wavulana ni **11938**.

Jumla ya vituo vya kufanyia mitihani ni **383** ikiwa vituo **370** ni vituo kwa ajili ya mitihani ya Kiswahili na vituo **13** ni kwa ajili ya mitihani ya Kiingereza ikiwa sawa na mikondo **1,217**.

Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Rukwa inawatakia kila la kheri wanafunzi wote wa darasa la saba Mkoani Rukwa na Tanzania kwa ujumla katika mitihani yao ya kumaliza elimu ya msingi na kuwaomba wafanye vyema huku wakizingatia taratibu zote za mitihani

Imetolewa na

A handwritten signature in black ink, appearing to read 'Khadija Dalasia'.

Khadija Dalasia

**Kaimu Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini**

**Mkoa wa Rukwa**

**10 Septemba 2024**